



07TH SEPTEMBER 2022

Tanganyika  
Law Society



# WAKILI SACCOS LIMITED

1. Bodi ya WAKILI SACCOS LIMITED inakaribisha maombi ya kujiunga na WAKILI SACCOS LIMITED iliyosajiliwa tarehe 16 May, 2022 chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika No. 6 ya mwaka 2013 na yenye usajili No. DSR 1795.
2. Wanachama wanaoweza kuleta maombi ni wale walio katika fungamano kwa mujibu wa Aya ya 4(i), (ii) na (iii) ya Masharti ya Chama.
3. Kwa mujibu wa Aya namba 11 ya Masharti ya Chama, maombi yatatumwa kupitia fomu Maalumu na iwapo maombi yatakubaliwa atapaswa kulipa malipo yafuatayo katika account ya WAKILI SACCOS No. 0133682683800 iliyopo CRDB Bank, Mlimani City Branch.
4. Malipo ya kujiunga uanachama ni pamoja na;
  - i. Kiingilio (kinalipwa mara moja) Tshs 100,000/= (Aya namba 13(1)(a) ya Masharti ya Chama).
  - ii. Hisa; Idadi ya hisa ni 10 zenye thamani ya Tshs 20,000/= kila moja, ambazo hisa 5 zinalipwa baada ya maombi ya uanachama kukubaliwa na hisa 5 zinalipwa ndani ya miezi matatu baada ya maombi ya uanachama kukubaliwa (Aya namba 13(1)(b) ya Masharti ya Chama).
  - iii. Kitambulisho (kinatolewa mara moja) Tshs 20,000/= (Aya namba 11(e) ya Masharti ya Chama).
  - iv. Gharama ya Fomu Tshs 10,000/= (Aya 23(a) ya Masharti ya Chama).
  - v. Hisa za hiari - zinanunuliwa muda wote - (Aya 27(2) ya Masharti ya Chama).
  - vi. Akiba ya kiwango chochote kisichopungua Tsh. 10,000/= kwa mwezi (Aya 13(1)(c) ya Masharti ya Chama).
5. Tafadhali zingatia kusoma vigezo na masharti ya Chama kabla ya kuomba uanachama.

